



**MADA: MIUNDO KATIKA KISWAHILI MIAKA 82 TANGU  
USANIFISHAJI (SWAHILI SYNTACTIC STRUCTURES 82 YEARS  
SINCE THE START OF STANDARDISATION PROCESS)**

Y. M. Kihore

kihore@udsm.ac.tz

Katika miaka ya karibuni na pengine hata katika miaka hiyo ya mwanzo, usanifishaji wa Kiswahili ulihusishwa zaidi na orodha rasmi ya maneno (kama msamiati na istilahi). Lakini wengine watakumbuka kwamba usanifishaji wa miundo ya sentensi ulifanyika pia katika maandishi mbalimbali yaliyochapishwa hasa yale yaliyoonekana yanaweza kutumika katika shughuli rasmi kama vile elimu, n.k. Kwa hivi leo suala la usanifishaji wa miundo ya sentensi hausikiki sana; na malalamishi yamekuwepo kuhusu kuingia kwa miundo ya lugha za kigeni na miundo mingine ambayo ukubalifu wake si wa moja kwa moja kwa wasemaji wengi. Miundo ya sentensi huhusishwa pia na ukweli kwamba utungaji wake hauna kikomo. Nia yetu katika makala ni kufuatilia historia ya usanifishaji wa miundo (kama umekuwepo kidhati) na mafanikio, changamoto au matatizo yake katika Kiswahili.

In more recent times and even much earlier, Swahili standardization has been more related to a list of formal word forms (as vocabulary and terms). However, as some of us may recall, standardization of Swahili sentences was also carried out in various publications, especially those intended for formal usage. Of late the process of standardization of Swahili sentences is not heard of much, although there are complaints here and there of unacceptable foreign or other structures in Kiswahili. We intend in this paper to trace the history of Swahili sentence structures (if it has ever been a serious undertaking) to determine its successes, challenges and/or problems.